**HOTUBA YA MGENI RASMI MHESHIMIWA ZELOTE STEPHEN ZELOTE MKUU WA MKOA WA RUKWA WAKATI WA KUFUNGUA MKUTANO WA UZINDUZI WA MRADI WA UIMARISHAJI MIFUMO YA SEKTA ZA UMMA MKOA WA RUKWA (PUBLIC SECTOR SYSTEMS STRENGTHERNING – PS 3) KWA AWAMU YA PILI TAREHE 15 MEI, 2017**

**Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya,**

**Mstahiki Meya wa Halmashauri ya manispaa ya Sumbawanga,**

**Mheshimiwa Mwenyekirti wa Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi,**

**Wakurugenzi wa Halmashauri,**

**Makatibu Tawala wa Wilaya,**

**Ndugu Kiongozi wa timu ya Mradi.**

**Wageni kutoka Taasisi zilizoalikwa,**

**Wajumbe wa Sekretarieti ya mkoa,**

**Wajumbe wa Timu ya Menejimenti kutoka kwenye Halmashauri,**

**Wanahabari,**

**Mabibi na Mabwana.**

Ni vyema wote tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana leo tukiwa na afya njema ambayo pia itawezesha shughuli hii ya mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma kuendeshwa katika Mkoa wa Rukwa.

Nimefarijika sana kupewa heshima ya kuwa mgeni rasmi katika ufunguzi wa mafunzo haya yenye lengo la kuwajengea uelewa wa yale yote yaliyopo katika mradi huu wa PS 3. Lakini la muhimu zaidi ni hili la kuwaleta pamoja jambo ambalo sio la kawaida na ningependa sasa kupitia mradi huu kadri fursa zinapotokea.

Katika mafunzo haya wapo pia Wakurugenzi wa halmashauri, Makatibu Tawala, Wajumbe wa Sekretarieti ya Mkoa na Wakuu wa Idara toka kwenye Halmashauri hizi mbili ambazo zinashiriki katika mafunzo haya. Hii ni ishara

kwamba mfumo huu wa PS 3 matakwa yake ni utekelezaji wa pamoja.

***Ndugu Washiriki,***

Nipende kuchukua nafasi hii vile vile kutoa shukrani za dhati kwa Serikali ya Watu wa Marekani ambao ndio wafadhili wa mradi huu kupitia Shirika la Kimaendeleo la Marekani (USAID) ambao wamefanya Mkoa wa Rukwa kuwa miongoni mwa Mikoa 13 itakayonufaika na mradi huu. Nawakaribisha wataalamu wote watakaohusika na kutoa mafunzo.

***Ndugu washiriki,***

Mradi huu wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta ya Umma umekuja katika wakati muafaka. Wote tunazifahamu na kuendelea kuzifuatilia jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali yetu chini ya uongozi wa Rais wetu Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, kuhakikisha kwamba serikali inahudumia wananchi ipasavyo, na kwamba

mifumo iliyopo serikalini inakuwa na tija kwa ajili ya kumsaidia mwananchi wa nchi hii.

***Ndugu washiriki,***

Ili tuweze kutekeleza kazi za serikali za kuhudumia wananchi kwa ufanisi ni lazima tuwe na mifumo imara. Nimwambiwa kwamba mradi huu utalenga kuimarisha mifumo ya: Utawala Bora na Ushirikishwaji wa wnanchi, Rasilimali watu, Fedha, mifumo ya Mwasiliano na Utafiti Tendaji. Haya ni maeneo muhimu ambayo bila shaka yakifanyiwa kazi vizuri yatazipa Halmashauri zetu uwezo wa kumhudumia mwananchi kwa ufanisi zaidi kwani upatikanaji wa huduma bora za serikali ni haki ya kila raia wa nchi hii.

***Ndugu washiriki,***

Uwepo wenu watendaji kutoka katika halmashauri zetu ni muhimu katika utekelezaji wa mradi huu. Ninyi ndio tunaowategemea kutekeleza shughuli za serikali katika maeneo

yenu, na ninyi ndio wenye mawasiliano ya moja kwa moja ya wananchi wa kawaida. Napenda kutoa rai kuwa hakikisheni kwamba mnatoa ushirikiano wa kutosha na kufanya kazi bega kwa bega na wataalam wanaouendesha mradi huu wa Uboreshaji Mifumo ya Sekta za Umma. Tunatakiwa kufahamu kwamba huu mradi ni wa kwetu na ni kwa manufaa ya nchi yetu, hivyo kuwajibika na kuhakikisha kwamba unakuwa na mafanikio makubwa ni wajibu wetu.

***Ndugu washiriki,***

Ni matarajio yangu kwamba wote tuliopo hapa tunajua tunao wajibu wa kuitekeleza sera ya Hapa Kazi Tu. Hivyo ni kazi yetu sisi viongozi wa Mkoa, Wilaya na Halmashauri kuhakikisha kwamba tunaitekeleza sera hiyo kwa vitendo, na kuhakikisha kwamba mifumo tuliyonayo inaboreshwa na maendeleo yanapatikana.

***Ndugu washiriki,***

Kwa kuzingatia maelekezo ya Katiba, Sera na Sheria za Serikali za Mitaa Halmashauri ni chombo cha wananchi cha kupanga, kutekeleza na kusimamia shughuli za kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiulinzi katika eneo husika. Madhumuni makubwa ya halmashauri yameelezwa katika Ibara ya 146 ya Katiba na Sheria za Serikali za Mitaa, majukumu hayo ni:-

i. Kuwashirikisha wananchi katika mipango na shughuli za utekelezaji wa maendeleo katika sehemu zao,

ii. Kuhakikisha utekelezaji wa ulinzi wa wananchi,

iii. Kuimarisha demokrasia katika eneo,

iv. Kuitumia demokrasia katika kuleta maendeleo.

***Ndugu washiriki,***

Katika kuhitimisha nasisitiza masuala yafuatayo:-

i. Ufuatiliaji na tathmini ya miradi inayotekelezwa
   - Sote tunashuhudia kuongezeka kwa fedha zinazopelekwa kwenye mamlaka za Serikali za Mitaa kutoka Serikali Kuu na makusanyo ya Ndani,

   - Fedha hizi hutumika pia kwenye utekelezaji wa miradi ya kisekta. (Elimu, Afya, Maji, Barabara na mengineyo),

   - Usimamizi na ufuatiliaji (Monitoring and Evaluation) unatakiwa kufanyika.

ii. Ukusanyaji, Usimamizi na Udhibiti wa mapato ya Ndani ya Halmashauri
   - Watumishi wote katika Mamlaka za Serikali za Mitaa wafanye kazi kwa juhudi na maarifa na pia waepuke kufanya kazi kwa mazoea ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato,

- Vyanzo vyote vya mapato vitambuliwe na Halmashauri zote zihakikishe kuwa kile kilichokusanywa kama ilivyokusudiwa ili kuongeza wigo wa ukusanyaji mapato,

- Wakurugenzi wa halmashauri zote wasimamie vizuri ukusanyaji wa mapato,

- Pamoja na majukumu mengine jukumu la kuongeza wigo na ukusanyaji wa mapato ndilo litakalokuwa kigezo kikuu cha kupima utendaji kazi wa Mkurugenzi.

iii. Uendeshaji wa shughuli za Halmashauri kwa misingi ya Utawala Bora

- Kushirikisha wananchi katika maamuzi,

- Kuwa na mshikamano kwa maana (Team work Spirit) kati ya wadau wote wa maendeleo ya Halmashauri,

- Kuepuka itikadi za vyama vya siasa katika kufikia maamuzi,

- Tukumbuke maendeleo hayana vyama.

Ndugu washiriki,

Baada ya kusema haya sasa natamka rasmi kuwa mafunzo haya yamefunguliwa.

Zelote Stephen Zelote

**MKUU WA MKOA WA RUKWA**